

UTANGULIZI

'Vita dhidi ya ugaidi' vilivyotangazwa baada ya septemba 11 mwaka wa 2001, haviwezi kufaulu kwa sababu vita vyenyewe vinatisha kwa hiyo vitaleta ugaidi zaidi. Miaka sita baadaye tunaishi katika dunia ambamo kuua na kuuliwa yamekuwa mambo ya kila siku na umuhimu wa maisha ya mwanadamu unarudi chini kila mara. Kuna njia za kutia wasiwasi za kujaribu kutatua kila vurugu kwa njia ya lazima.

Umuhimu wa ukristo

Kama wakristo, tunakubali kwamba tangu siku za mfalme konstantino, dhuluma na nguvu za majeshi zimetumika na wakristo. Uweza wa sasa wa hali ya juu katika uchumi na majeshi katika mataifa yaliyostawi ya magaribi unaaminika kutokana na ukristo katika mataifa mengine duniani. Shirika la NATO linaaminika kuwa kundi la kikristo linalojiingiza duniani kote na kuzusha vita kwa masilahi yake. Na sasa kundi la wanaharakati la dini ya pili katika ukubwa duniani ikiwa uislamu linajitetea kwa kuzishambulia nchi za magharibi zisizomwamini Mungu kwa njia mpya za kivita kama mabomu ya kujilipua.

Kazi ya kanisa la kikristo.

Ujumbe wa agano la kale na agano jipya unaweza ukatajwa kwa kifupi kama ifuatavyo; Mungu amewachagua watu wa Israeli, Yesu wa Nazareti na kanisa la kikristo kuwa baraka duniani. Kuinuka kwa kanisa la kikristo ambako hakuwezi kusimamishwa kama shirika lisilo na silaha na lisilo la kiserakali kulitokea kwa sababu ujumbe wake wa heshima na haki za kila mwanadamu uliwashawishi watu zaidi na zaidi. Yesu alifunza kwamba Mungu anawapenda hata wasiomwamini, na kwamba uovu hauwezi kushindwa na uovu. Aliyatoa maisha yake kwa msimamo huu. Tunauliza katika sala ya Bwana kuwa ufalme wa Mungu uje na dhambi zetu zisamehewe na tuko tayari kuwasamehe wale watutendeao dhambi. Je, tumesahau kwamba sisi wenyewe tunahitaji kukombolewa kutokana na uovu?

Kuiacha njia isiyo sawa.

Njia mbaya ya ukristo na uharibifu wa injili inaonekana wazi wakati wakristo wenyewe wanapanga ama kuingizwa katika mapambano ya mauaji dhidi ya binadamu wenzao na kutishia kuangamiza walimwengu {jamii ya wanadamu}. Je, vita vinaweza kuwa na haki yoyote? Je, kuwaua wanadamu wengine kunaweza kuwa sawa? Inawezekana kuzibadili njia zetu. Wakristo wengi wanajitahidi kuondosha desturi za chuki na hofu kwa njia za amani. Vile vile, watu wengi wa imani nyingine na mashirika yasiyo ya kiserikali duniani yamegundua kwamba njia zetu za sasa haziwezi zikaendelea kutumika. Wamejitolea kuwapa watu waliokata tama matumaini mapya na ujasiri wa kukabili maisha. Na hata licha ya jitihada hizi, hatari ya walimwengu inaendelea kukua. Kwa nini?

Kushinda uanajeshi.

Hata katika mwanzo wa milenia ya tatu tabia ya kale ya mwanadamu ya kujiwekea silaha za kupigana na adui inaendelea bila kupungua hata na matumizi ya silaha zilizo hatari zaidi. Watu wengi hawawezi kufikiri mwisho wa hali hii. Wakristo wasiwe watu wa kushindwa sana. Katika harakati za amani miaka ya 1980s, wengi walikubali ahadi ya unabii. 'nao watafua panga zao ziwe majembe, wala hawatajifunzavita tena kamwe'. {Isaya

2:4,Mika 4:3}.Vita hupiganwa na wanadamu na pia vinaweza vikakomeshwa nasi.Tukumbuke ombi la umoja wa mataifa baada ya vita vya pili vya ulimwengu`kuokoa vizazi vijavyo kutokana na pigo la vita'lengo letu ni `tusijifunze vita tena'.Kinachohitajika katika dunia hii si ujasiri wa kuhatarisha maisha kwa kumwagamiza adui ama kujitoa mhanga kwa kujilipua ukitumia bomu.Kinachohitajika ni ujasiri wa Yesu,ujasiri wa waume na wake wa kawaida ambao ni heri wafe wao wenyewe badala ya kuwaua wanadamu wenzao.Takwimu za mwisho za shirika la kimataifa la utafiti la Amani la Stockholm linaonyesha kuwa katika mwaka wa 2006,Dola za kimarekani bilioni 1204,zilitumika duniani kote kwa ununuzi wa silaha za vita.Tunadai pesa hizi zipelekwe katika kusaidia mashirika ya kusaidia raia yanayofanya kazi kwa njia ya amani,haki na kuhifadhi ardhi.Tunainua sauti zetu na kutangaza;`Hatuna imani katika dhana kwamba nguvu za kijeshi zinazotumiwa kuwaumiza wengine zinaweza kutulinda kwa muda mrefu.'Tunainua sauti zetu na kudai kuwa na mabadiliko ya mtazamo katika serikali zetu.Tunazitarajia zijiitolee kuendeleza sera za kushinda vita na kufuatilia kwa kina lengo hili.

Ushirikiano kwa sababu ya Amani.

`Sauti hizi kutoka Schorndorf'zinatolewa kusaidia miradi ya Shirika la makanisa Duniani katika muongo wa kukabiliana na vurugu, 2001-2010.Shirika hili linayaleta pamoja makanisa yote duniani kwa sababu ya amani.Juhudu hizi zitakamilishwa na uundaji wa sheria ya tangazo la ulimwengu wote la `Amani ya haki'katika kusanyiko la mataifa yote duniani mnamo mwaka wa 2011.

Tunataka lengo la `kutojifunza vita tena'lihusishwe katika azimio hilo la amani.Tunawauliza `wakristo wote'kujiunga na`Sauti hizi kutoka Schorndorf'na kuzisukuma serikali zao na kuunga mkono miradi ya amani ya shirika la Makanisa Duniani.